**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 03 Machi, 2022**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**
Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:**
Hotuba ya maoni ya Kamati ya Uchumi Kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

## III. MASWALI:

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

99. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

    Katika kipindi cha karibu miezi tisa hali ya upandaji wa bei za chakula na vifaa vya ujenzi imekuwa ya kutisha, hali hii inawaumiza na kulalamikiwa sana na wananchi hali ambayo sio nzuri katika utulivu wa nchi.

(a) Je, ni hatua gani zinazochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na tatizo hilo la upandaji wa bei kwa bidhaa muhimu.

(b) Kwa kuwa Serikali imeweka mifumo ya utoaji wa ruhusa wa uagiziaji wa bidhaa "monopoly" Je, mfumo huo hausababishi upandaji wa bei.

**Wizara ya Maji, Nishati na Madini:**

65. MHESHIMIWA SULUBU KIDONGO AMOUR (Jimbo la Mkwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Tunaipongeza Serikali kwa kuleta shughuli za uwekezaji katika visiwa vya Zanzibar kwa ajli ya kupata maendeleo ya wananchi wake. Hata hivyo, wawekezaji hao wanakabiliwa na ugumu wa kufanya kazi kutokana na kukosa maji na umeme wakati wa shughuli hizo zikiendelea.

Serikali kupitia Wizara husika inasimamia vipi shughuli za uwekezaji kwa wawekezaji kupitia miundombinu ya maji na umeme ili kusiwe na kipingamizi cha utekelezaji wa kazi zao.

133. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Katika shehia ya Mtangani jimbo la Kiwani, kuna kijiji cha Kichaka na Chwaka ambavyo vilikuwa vikipata maji ya bomba kutoka Kendwa, lakini kwa bahati mbaya muda mkubwa hawapati huduma hiyo.

(a) Je, Mhe. Waziri tatizo hilo unalifahamu.

(b) Je, Wizara ina mkakati gani wa kuwapatia wananchi hao huduma hiyo ya maji.

**Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:**

154. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Pamoja na kwamba Serikali ilijenga jengo la Kituo cha Afya Maziwani ndani ya jimbo la Pandani tokea mwaka 2012, hadi sasa hakuna huduma yoyote inayotolewa kituoni hapo.

(a) Je, ni lini Serikali itakizindua rasmi kituo hicho na kuanza kutoa huduma kwa wananchi wa Maziwani, Shengejuu na vijiji vyengine ambavyo vituo vya afya viko mbali nao.

(b) Kwa vile barabara ya kukifikia kituo hicho ni mbaya sana, ni upi mpango wa Serikali wa kuwapatia wananchi wa kijiji cha Maziwani usafiri wa dharura wa wagonjwa unaoendana na barabara hiyo wakati jitihada za kuitengeneza zikiendelea.

(c) Je, ni wafanyakazi wangapi wenyeji wa jimbo la Pandani wameajiriwa kutoa huduma katika kituo cha afya cha Maziwani.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

129. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika vipaumbele vya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2021/2022, ni kuzipatia skuli zote za maandalizi, msingi na sekondari ruzuku za uendeshaji na vifaa vyenginevyo vikiwemo vya maabara.

(a) Je, Mhe. Waziri lengo hili limetekelezwa kwa kiasi gani.

(b) Je, ni kiasi gani cha ruzuku mpaka sasa kimeshatumika.

157. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kama ilivyo kawaida kwa Serikali, kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, iliahidi kusaidia ujenzi wa skuli ya maandalizi ya Mwane iliyomo ndani ya jimbo la Pandani. Hata hivyo, tokea wananchi kujenga na kufika hatua waliyofikia, Serikali haijaikaguwa tena skuli hiyo ambayo imeanza bila maji, umeme

na vyoo, hali ambayo si salama kwa afya za watoto na walimu wao.

(a) Je, ni kwa nini Serikali haikutimiza ahadi yake hiyo kwa wananchi wa Mwane ndani ya jimbo la Pandani.

(b) Je, ni lini Serikali itafanya ukaguzi wa skuli ya maandalizi ya Mwane ndani ya jimbo la Pandani.

(c) Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake kwa kukamilisha mapungufu yaliyopo sasa katika skuli ya maandalizi ya Mwane ili ikidhi vigezo vya awali vya skuli za msingi.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

48. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Wasafiri wanaotumia usafiri wa boti katika Bandari ya Dar es Salaam na Zanzibar wanatakiwa kuonyesha vitambulisho vyao kwenye bandari zote mbili kwa safari moja, hali ambayo inaleta usumbufu mkubwa kwa wasafiri hao.

(a) Je, kwa nini Serikali isipange utaratibu wa kuangalia vitambulisho hivyo wakati wa kuingia tu kwenye chombo kama ulivyo usafiri wa boti.

(b) Je, ni hatua gani ambazo huchukuliwa kwa abiria ambaye atashindwa kuonesha kitambulisho chake wakati ameshateremka kwenye boti.

50. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini)- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika kukabiliana na wimbi la uhalifu na utapeli kupitia mitandao ya simu, Serikali kupitia Mamlaka ya TCRA iliagiza kwa kampuni zote za simu kutokufanya usajili wowote wa namba ya simu bila muhusika kuwasilisha kitambulisho chake. Hata hivyo hadi leo wapo watu wanaotumia namba ambazo hazikusajiliwa kwa majina yao na hivyo kuendelea kutapeli na kufanya uhalifu.

(a) Kwa kuwa agizo hili ni la muda mrefu, na kwa kuwa hadi sasa wapo watu ambao wanatumia laini ambazo si za majina yao, Je, Serikali inawaahidi nini wananchi.

(b) Ni hatua gani za kisheria zinaweza kuchukuliwa dhidi ya kampuni za simu zinazokaidi agizo hilo.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**
Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo – Kusomwa kwa mara ya Pili.

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**03 Machi, 2022.** **KATIBU WA BARAZA.**